# GRETSA UNIVERSITY - THIKA

## UNIVERSITY EXAMINATIONS
## JANUARY-APRIL 2025 SEMESTER

## BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

**KODI: KISW 202**
**KOZI: FONETIKI NA FONOLOJIA YA KISWAHILI**

**TAREHE: APRIL 2025** **WAKATI: 2 HOURS**

---

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MAWILI**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTIHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. ANDIKA VIDOKEZO VYAKO **NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU** KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE

***TAHADHARI**:-kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani*

**SEHEMU YA A: YA LAZIMA**

**SWALI LA KWANZA**

**a)** Andika maneno yafuatayo kwa kutumia Alama za IPA:

- **i.** Njia **[Alama 2]**
- **ii.** Sheshe **[Alama 2]**
- **iii.** Changanya **[Alama 3]**
- **iv.** Kioo **[Alama 2]**

**b)** Bainisha taarifa muhimu tunazozipata kuhusu sauti za lugha zilizomo katika jedwali la IPA. **[Alama 4]**

**c)** Eleza sifa nne za fonimu. **[Alama 4]**

**d)** Andika sheria ifuatayo ya kifonolojia kwa kutumia sifa bainifu za fonimu husika: **[Alama 4]**

/b/ ⟶ [z]/ - /i/ ya unominishaji

**e)** Tambua sababu mbili za kuwakilisha sauti za lugha kwa kutumia Alama za IPA. **[Alama 4]**

**f)** Fafanua tofauti na mwingiliano uliopo kati ya taaluma za fonetiki na fonolojia. **[Alama 5]**

---

**SEHEMU YA B: YAJIBU MASWALI YOYOTE MAWILI**

**SWALI LA PILI**

**a)** Bainisha sifa bainifu za kifonetiki za vipasuo sita katika Kiswahili. **[Alama 12]**

**b)** Eleza majukumu ya alasauti zifuatazo katika utamkaji wa sauti za lugha:

- i. Ulimi **[Alama 2]**
- **ii.** Kongomeo **[Alama 2]**
- **iii.** Kilimi **[Alama 2]**
- **iv.** Kidakatonge **[Alama 2]**

**SWALI LA TATU**

**a)** Jadili vigezo vitatu vinavyotumiwa kuainisha vokali. **[Alama 12]**

**b)** Fafanua mfumo wa kuweka mkazo katika Kiswahili Sanifu. **[Alama 8]**

**SWALI LA NNE**

**a)** Eleza mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia:

- i. Ukaakaishaji **[Alama 5]**
- **ii.** Kuimarika kwa sauti **[Alama 5]**
- iii. Kudhoofika kwa konsonanti **[Alama 5]**

**b)** Bainisha sifa tatu za alofoni. **[Alama 3]**

**c)** Dhihirisha mifano miwili ya alofoni katika Kiswahili Sanifu. **[Alama 2]**

**SWALI LA TANO**

**a)** Fafanua mitazamo miwili kuhusu dhana ya fonimu. **[Alama 10]**

**b)** Bainisha miundo mitano ya silabi katika Kiswahili Sanifu. **[Alama 10]**